MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 6 TOLEO 24

JANUARY 27, 2009

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

MAKALA MAALUM

KASHFA YA EPA

LA KAGODA SI GUMU

NANI ALICHUKUA FEDHA BENKI?



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Na. Fred Katunzi



Dalili zinaonesha kuwa wahusika wa kampuni inayotuhumiwa kuchota zaidi ya bilioni 40 kutoka katika Akaunti ya Masalio ya Madeni ya Nje (EPA) ya Kagoda ni vigumu kuwapata licha ya ukweli wote kuwa hadharani kuhusu wahusika hao.

Tunaamini kabisa kuwa wahusika hawa wapo, wanajulikana, na mbinu zozote za kujaribu kuwakwepa ni kuchezea utawala wa sheria, kujaribu kulizuga taifa na zaidi ya yote kujaribu kutengeneza kesi dhaifu dhidi yao.

Imani hii imethibitishwa wiki ili-



Mkuu wa BRELA Bw. Esteriano Mahingila

yopita pale ambapo habari kadhaa zilienezwa ambazo kimsingi zote zinakwepda kuuliza swali la msingi katika suala hili la Kagoda. Habari moja iliandikwa kwenye gazeti la Tanzania Daima ambapo lilidai kuwa "Kagoda njia nyeupe".

Kwa mujibu wa gazeti hilo chanzo chao kimoja cha habari kilidai kuwa "Wamiliki wa **(inaendelea Uk 2)**

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimerushusiwa!**

Ndani ya Toleo Hili

La Kagoda siyo gumu	1
Hoja ya Mwanakijiji	1,3
La Kagoda siyo gumu	2,3,4
Hoja ya Mwanakijij	4
Habari Mbalimbali	4,5
Da' Jessy: Tanzania yetu	5
Picha, Katuni na Maoni	6

HOJA YA MWANAKIJIJI — KAULI ZA WAZIRI MKUU NAZIKATAA

Nachukulia kauli za Waziri Mkuu Mizengo Pinda kuwa zimekuja kwa bahati mbaya. Kwa vile hazijakanushwa au kufutwa nachukulia kuwa alimaanisha alichosema.

Kwa kweli hana haki, nguvu, wala uwezo wa kutangaza adhabu kwa mtuhumiwa yeyote yule. Waziri Mkuu amenukuliwa na gazeti la Mwananchi la tarehe 23 mwezi huu akitangaza kuwa sasa serikali imechoshwa na hivyo kuruhusu watuhumiwa wa mauaji ya albino wakikamatwa nao wauawe.

Gazeti hilo lilimnukuu Mhe Pinda akisema kuwa "Mkimuona mtu akamkata



mwingine shingo naye muueni kwani sasa viongozi wote tumechoka... no more, I can't tolerate anymore (imetosha, siwezi kuvumilia tena). **(inaendelea Uk. 3)**

LA KAGODA SIYO GUMU HIVI

Kagoda wanajulikana lakini serikali haiwezi kuwakamata kwa kuwa hakuna ushahidi lakini pia wana siri nzito, ndiyo maana wizi wa nyaraka ulifanyika kwa kiwango cha juu" Gazeti hilo hilo lilimnukuu Waziri wa Katiba na Sheria Bw. Mathias Sikawe ambaye alidai kuwa "Serikali hatuwezi kufanya kazi kwa shinikizo la kisiasa, tunampeleka mtu au kampuni mahakamani kwa mujibu wa taaluma ya sheria na pia sisi si wapelelezi"

Wakati tunaendelea kutafakari habari hizo Afisa Mkuu wa Wakala wa Serikali wa Usajili wa Makampuni (BRELA) Bw. Esteriano Mahigila aliitisha mkutano wa waandishi wa habari ambapo alisema mambo makubwa mawili ambayo yote hayahusiani na swali kubwa zaidi. Alidai kwanza kwamba faili la Kagoda lipo na mtu yeyote anaweza kuliona na hakuna siri yoyote humo. La pili ni pale alipodai kuwa "wamiliki" wa kampuni hiyo wanajulikana na akawataja kwa majina ya kuwa ni Francis William na Johnson Kyomhando.

Kwa muda mrefu pia wapinzani wamekuwa wakijaribu kuelezea fedha za Kagoda zimeenda wapi ambapo wao wanadai kuwa fedha hizo zilitumiwa na CCM kwenye uchaguzi mkuu wa 2005. Madai hayo yamepigiwa mbiu sana na Mbunge wa Kigoma Kaskazini Mhe. Zitto Kabwe.

Katika haya yote tunaamini swali moja ambalo linaweza kabisa kujibu swali ambalo sisi tumeshalijibu kwenye matoleo yaliyopita halijajibiwa wala kutafutiwa majibu. Maswali ya "nani mmiliki wa Kagoda?" na "fedha za Kagoda zilitumika vipi" tunaamini ni maswali yasiyo sahihi katika kutafuta ukweli wa mwizi aliyechota bilioni 40 kutoka kwenye Benki yetu kuu.

Swali ambalo linahitaji kujibiwa ni hili nalo lina sehemu mbili zinazohusiana: "ni nani aliyekuja kuchukua bilioni 40 toka Benki Kuu?; sehemu ya pili "ni nani aliyepeleka fedha hizo kwenye benki mbalimbali nchini?" Kuna ushahidi wa kutosha kuwa mtu aliyechukua fedha Benki Kuu ndiye huyo huyo aliyezipitisha kwenye benki nyingine. Kumpata mtu huyo itakuwa ni kumpata mwizi wetu.

Swali hilo hata hivyo ndani yake linatuongoza kujenga hoja zifuatazo:

NAMES, ADDRESSES AND DESCRIPTIONS OF SUBSCRIBERS	NUMBER OF SHARES TAKEN BY EACH SUBSCRIBER	SIGNATURES
JOHN KYOMUHENDO P.O. BOX 80154 DAR ES SALAAM TANZANIA. DIRECTOR	40 SHARES	Kyomuhendo
FRANCIS WILIAM P.O. BOX 80154 DAR ES SALAAM TANZANIA. DIRECTOR	60 SHARES	

Dated at D' SALAAM this 28TH day of SEPTEMBER 2005

Witness to the above Signatures:

Name: BENJAMIN MWANGONDA
KHATCO MANAGEMENTS LTD.

Signature: MANAGEMENT & TAXATION CONSULTANTS
P.O. BOX 2291

Postal Address: DAR ES SALAAM

Qualification: ACCOUNTANT

a. Kwamba kiasi cha bilioni 40 zimechotwa toka Benki Kuu hilo halina ubishi. Kinachotusumbua ni kuwa kwa miaka karibu mitatu serikali yetu inajifanya kuwa haijua ni nani aliyezichota! Kwamba inawezekana mtu/watu wakapanga njama za kuiba toka benki kuu, wakafanikiwa kufanya hivyo, na kutoweka hewani kama moshi inatisha.

b. Aliyechukua fedha toka Benki Kuu ni wazi kuwa hakuingia huko kama mzuka wa aina fulani, ni mwanadamu ambaye anafungwa na sheria zote za fizikia. Ina maana kuwa mtu huyo aliweza kwenda benki kuu, alionekana na watu wanamfahamu. Mtu huyo siyo shetani.

c. Kwamba fedha zilizochukuliwa ni nyingi mno kiasi kwamba uwezekano kuwa haijulikani nani alizichukua ni kutukana akili za Watanzania. Ingekuwa imepotea ni Shs 500 basi hata kuuliza hatuwezi kwani inaweza kupotea hivi hivi, lakini zinapopotea bilioni 40 halafu hatujui nani kazichukua ni kejeli kwa watu wote wenye akili timamu. Sisi "Cheche" tunakataa mara moja na daima uwezekano huo.

Je tunaweza kupata majibu ya swali hilo? Tunaamini kwanza kabisa kuwa kuna watu watatu ambao wanashikilia ufunguo wa kujua ni "nani aliyechukua fedha toka Benki". Watu hao ni kwa mfuatano wa umuhimu wao ni Peter Noni ambaye ni shahidi wa upande wa mashtaka katika kesi kadhaa za EPA (huyu kwa sasa tunamuweka kiporo tukifuatilia kinachoendelea mahakamani). Wengine wawili ni Benjamin Mwangonda ambaye ni mhasibu kwenye kampuni ya Khatco.

Uchunguzi wetu unaonesha vitu kadhaa kuhusu Bw. Mwang'onda. Kwanza, ni mtu ambaye anaweza kabisa kusema ilikuwaje jina lake na sahihi yake kuwepo kwenye nyaraka za usajli wa kampuni ya Kagoda. Mhuri wa ofisi yake wenye maneno ya "Khatco Management"

(inaendelea Uk. 3)

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

umebandikwa. Kuwepo kwa jina lake na mhuri wa ofisi yake kunatupa mambo mawili tu ya kuchagua; kwanza, ni yeye aliyeshuhudia kina Francis William na Johnson wakitia sahihi hati hizo na bila ya shaka anawajua hawa ni kina nani. La pili siyo yeye aliyetia sahihi nyaraka hizo na mhuri huo licha ya kuwa ni wa ofisi yake kuna mtu mwingine aliyeutumia kwenye nyaraka za Kagoda.

Hadi hivi sasa taarifa zote ambazo tumezifuatilia kwa ukaribu hadi mwishoni mwa juma zinaonesha kuwa Bw. Mwang'onda hajahojiwa kuhusu Kagoda. Vyanzo vyetu vya kuaminika kabisa vinadokeza kuwa kampuni hii ya Khatco ndiyo inatumika katika shughuli za uhasibu katika mojawapo ya makampuni ya yule ambaye tulimtaja huko nyuma kuwa anahusika na kampuni hii Mhe. Rostam Aziz (CCM – Igunga). Huyu Mwang'onda ni mtu muhimu kutujulisha kuhusu usajili wa Kagoda.

Zaidi pia ni mtu ambaye ataeleza uhusiano wa kampuni ya Khatco na makampuni kadhaa ya Mhe. Aziz.

Mtu wa tatu ambaye ni muhimu katika kuijua Kagoda ni Mwanasheria Beredy Sospeter Maregesi. Mtu huyu ni muhimu kwanza kwa sababu iliyowazi kwamba jina lake linatajwa katika makampuni mawili ambayo yanatuhumiwa kuchota fedha za EPA. Makampuni hayo ni Maregesi Law Chambers na G&T International Ltd. Kwanini hadi sasa Bw. Meregesi hayafikishwa mahakamani? Jibu lake tunaamini liko kwenye sababu ya pili kwanini tunaamini mtu ambaye licha ya kushtakiwa kwa makosa yake yeye mwenyewe lakini pia anashikilia ufunguo wa kumwelewa ni nani aliyechukua fedha Benki kuu.

Sababu hiyo ni ile ambayo tuliandika katika toleo letu la 15, Juzuu ya 4 tarehe 25 Novemba, 2008. Tulieleza hivi kuhusu mpango wa wizi wa fedha za EPA ulivyosukwa "Gavana Ballali alihakikisha kuwa kunakuwa **(inaendelea Uk. 4)**

SWALI LA WIKI:

Je unafikiri katika kupambana na mauaji ya Albino tupinde sheria zetu na kuruhusu watu kujichukulia hatua mikononi dhidi ya wale wanaowatuhumu kuhusika na vitendo vya mauaji hayo au hata katika hilo sheria zetu lazima zifuatwe na watu watumie vyombo vya sheria kuwaadhibu wahusika?

Tuma majibu yako: mhariri@klhnews.com

Zaidi ya yote gazeti hilo lilimnukuu Bw. Pinda akiagiza umoja wa vijana kuwa "mna jeshi zuri ambalo naamini mkiamua mnaweza kutokomeza mauaji ya wazee wetu pmoja na ndugu zetu maalbno na kazi hiyo nawaagiza muanze leo msisubri auawe mwingine tena"

Katika kauli hizo mbili naweza kuona mambo mawili ambayo ningependa kuyaangaliza hapa. Kwanza inaonekana kweli Waziri Mkuu amechoshwa na mauaji haya na pili amependekeza suluhisho la hatari kukabiliana na mauaji haya. Waziri Mkuu amependekeza mauaji ya watu wengine katika kupinga mauaji ya watu wengine!

Mwandishi wa habari hiyo aliweza kabisa kuonesha tofauti ya kile ambacho Pinda alisema ni kile ambach Rais Kikwete alisema kwenye mojawapo ya hotuba zake. Rais Kikwete yeye alisema kuwa watu wanaoua albino wanastahili adhabu ile ile wanayopewa watu wengine kwa makosa ya kuua kwa kukusudia. Tofauti yao ni kuwa Rais Kikwete alizungumzia kama adhabu ya mahakama na Pinda alizungumzia kama hatua za raia kuchukua sheria mikononi.

Naamini kabisa kuwa Waziri Mkuu amesema haya yote kwa nia njema akisukumwa kweli na uchungu wa adha (plight) ya ndugu zetu maalbino ambao wamegeuzwa mawindo katika taifa lao. Yote hayo hata hivyo hayaondoi ukweli kuwa tukikubali kuwa watu waanze kuchukua hatua hizi mikononi tutakuwa tumehalalisha uvunjaji mkubwa wa sheria nchini.

Tukikubali kuwa watu wajichukulie sheria mikononi kwa sababu wamechoshwa na kero ya uhalifu fulani tutakuwa na tofauti gani na wale wanaokamata vibaka Kariakoo na kuwatia viberiti? Tutakuwa na tofauti gani na wale ambao wanamkamata mwizi wa kuku na kumpiga hadi kumuua wakati kituo cha Polisi kipo karibu?

Tunapotaka watu waheshimu utawala wa sheria hatuna maana wawe na hiari ya kuheshimu utawala wa sheria. Katika nchi ya kidemokrasia (au inayojaribu kujenga demokrasia) sheria ndiye dikteta! Pinda kama vile alivyo James na kama vile alivyo Zeituni wote wanabanwa na sheria. Haiwezekani yeye mwenzetu kutoa maagizo ambayo anafikiri ana uwezo wa kuyatoa kwa sababu yuko "nje" ya sheria. Hili ni la kupinga.

Mtu mwingine anaweza kuchukulia kuwa mwanakijiji aone mauaji haya ndivyo atajua kwanini hatuwezi kuchezea suala hili. Ukweli ni kuwa mimi ni miongoni mwa watu ambao kwa mwaka mzima tumetoa mapendekezo kadha wa kadha ambayo hayajatekelezwa, mapendekezo ambayo naamini yanaweza kabisa kupunguza na kutokomeza mauaji haya. Nimeandika tena kwenye gazeti la Tanzania Daima la kesho na kutoa mapendekezo ya jinsi gani kama taifa tunaweza kupambana na aibu hii.

La mwisho ambalo pia ni la kupinga ni kauli ya Waziri Mkuu kutaka UVCCM kushiriki kama "jeshi" kupambana na mauaji ya Albino. Kwa vile hadi sasa Waziri Mkuu hajafuta kauli hizo naamini kabisa kuwa ni za kweli. UVCCM siyo jeshi na wao kushiriki kufanya kazi ya jeshi au kwa namna yeyote ile kujichukulia sheria mikononi ni makosa ambayo natumaini DPP hatochochelewa kuyafuatilia.

Hata kuwaagiza Sungusungu ambao kwa watu wa kanda ya ziwa wanajua sifa yao ni kuchezea maisha ya wote. Hawa Sungusungu hawana mafunzo yoyote ya kipolisi au ya masuala ya haki za binadamu. Endapo Sungusungu hawa wakitekeleza maagizo ya Waziri Mkuu wakafanya mauaji makubwa huko tunajua wazi ni nani wa kumlaumu. Haitoshi kutuambia kuwa Waziri Mkuu "alimaanisha" nini, wakati wale waliomsikia wanajua ni nini hasa alimaanisha.

Kama tumeshindwa na Polisi, tumeshindwa na JWTZ, tumeshindwa na TISS na vyombo vingine vya usalama, kama kweli tumeshindwa kutokomeza mauaji haya kwa kutumia mbinu za kisasa na sasa tumekimbilia ulinzi wa jadi (wakati waganga wa jadi tumewafutia leseni) hatuna budi kujiuliza kama tunaongozwa na akili zetu au hisia zetu. Kama Waganga wa Jadi tumewafutia leseni, hawa Sungusungu tunaowapa jukumu la kuingilia hata uhai wa watu wana leseni gani ya ulinzi? Ni maafisa wa jeshi gani hawa? Je wakifanya makosa watashtakiwa kwa "police code" gani?

Ninachosema ni kuwa kauli hizi za Waziri Mkuu kama zinavyoendelea kusimama zilivyo (inaendelea Uk. 4)

Soma bure

LA KAGODA SI GUMU HIVYO

na makubaliano kati ya watu wa Mkapa na Benki Kuu na akaandika kila kitu na makubaliano hayo yana nguvu ya kisheria" anasema mchunguzi wetu. "Hata hivyo makubaliano hayo yanawaumiza watu kichwa; inajulikana nakala ya makubaliano hayo ipo kwa Maregesi (Mwanasheria aliyehusika na pia kunufaika na fedha za EPA) na Bi. Komu (mtumishi wa Benki Kuu). Lakini pia mtu mwingine anayejua kilichofanyika upande wa Benki Kuu ni Bw. Mwakosya"

Taarifa ambazo tumeendelea kuzipata kutoka vyanzo vyetu vya uhakika vimethibitisha taarifa hizo za awali. Kuna kile kinachotajwa kuwa ni usia wa Gav. Ballali ambao watu kadhaa wanajua kilichoandikwa ndani yake. Kwa mujibu wa vyanzo hivyo Bw. Peter Noni na Maregesi ni miongoni mwa watu wachache wanaojua ni nani hasa waliochukua fedha za EPA kwa kutumia kampuni ya Kagoda.

Tunaamini suala la Kagoda halihitaji kitu chochote nje ya vile ambavyo tuna uwezo navyo; bali linahitaji ujasiri wa "liwalo na liwe".

Ujasiri huo utaanza kwa kuwataja wale wafanyabiashara wawili walioshirikiana kuchukua fedha Benki, na kwa pamoja kuzipitisha kwenye akaunti mbalimbali. Tunawajua, kazi iliyopo ni kwa serikali kusema kama inaweza kuwataja bila kujali gharama yake.

Endapo serikali inaona kuwa haiwezi aidha kwa sababu ya woga, aibu, au kuoneana huruma kuwataja na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika basi ni bora iseme wazi ili angalau wananchi tujue kuwa serikali yetu imeshindwa na tuendelee na masuala mengine.

Vinginevyo kama alivyosema Dr. Mwakyembe siku ya Jumapili mashtaka ambayo yameletwa hadi hivi sasa kwenye kesi hizi nyingi (ikiwemo ya Richmond) ni mashtaka mepesi sana.

Sisi kama yeye tunaamini serikali itapitia tena ushahidi wote uliopo na kuyabadilisha mashtaka hayo ili yaendane na uzito wa makosa yanahodaiwa kutendwa. Katika kufanya hivyo wahusika wote watashughulikiwa kisheria.

CCM YASHINDA MBEYA, JAJI MAKAME ASEMA HAKUNA MCHEZO MCHAFU

Na. Mwandishi Wetu

Matokeo ambayo yamepatikana jana jioni kutoka vituo mbalimbali yanaonesha kuwa Chama cha Mapinduzi kimeweza kutetea Jimbo la Mbeya Vijijini na kuziba nafasi iliyoachwa wazi kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo miezi mitatu hivi iliyopita Bw. Richard Nyaulawa.

Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Taifa Jaji Lewis Makame amesema kuwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi (Assistant Return Officer) Bi. Fidelian Mkomola hakukosea pale alipohifadhi masanduku ya kupigia kura nyumbani kwa wifi yake ambapo ni karibu na kituo cha kupigia kura.

"Alifanya uamuzi sahihi kwani nyumba hiyo ni ya wifi yake na sheria haisemi ayatunze wapi masanduku hayo bali ahakikishe yapo salama" alisema Jaji Lewis alipozungumza na shirika la Utangazaji la Uingereza BBC katika matangazo yake ya jana jioni.

Bi. Mkomola alituhumiwa na uongozi wa CUF wa kukutwa na masanduku hayo kwa kile ambacho kilidaiwa kuwa ni "mchezo mchafu".

Hata hivyo Jaji Makame alishangazwa na tuhuma hizo kwa kusema kuwa "kabla ya kupiga kura masanduku yote hufunguliwa mbele ya wawakilishi wa vyama na waandishi wa habari, sasa mchezo gani hapo". Chama cha CUF hata hivyo kimeonesha dalili ya kutoridhika na matokeo hayo.

HOJA YA MWANAKIJIJI: NAZIKATAA KAULI ZA WAZIRI MKUU



siyo za kupuuzwa au kuzichukulia kwa urahisi ni kauli za kulaani na za kuweza (kwenye nchi zinazoheshimu kweli utawala wa sheria) kumlazimisha hata Waziri Mkuu kujiuzulu. Waziri Mkuu aombe radhi kwa kauli hizi na kama anazisimamia basi aachie ngazi ili mtu mwenye kutaka kulinda kweli sheria zetu ashike nafasi yake.

Kwa mtindo huu wa kujaribu kuongozwa na jaribu na matatizo ya wakati fulani na hivyo kulazimika kufanya vitu nje ya sheria inanikumbusha Waziri Mkuu mwingine ambaye naye alikuja na kisingizio hicho hicho na kuamua kufanya vitu nje ya sheria. Sasa hivi na yuko nje ya serikali. Nitasikitika kama Pinda naye ameingia kwenye mtego huu wa kuanza kulewa madaraka.

Hapa nitumie maneno ya Rais Barack Obama siku ya kuapishwa kwake akizungumzia suala la usalama wa Marekani. Bw. Obama alisema kuwa "tunakataa kwani ni uchaguzi wa uongo kati ya usalama wetu na tunu zetu tunazoshikilia".

Hili na sisi Watanzania tulikatae. Uchaguzi uliowekwa mbele yetu na Waziri Mkuu ni wa aina hiyo. Kwamba aidha tufuate sheria zetu na kushughulikia wahusika wa vitendo hivi vya kinyama katika vyombo vyetu au tuwashughulia papo kwa papo. Huu ni uchaguzi wa uongo.

Tumezazaliwa kama taifa linalosema kila binadamu anastahili haki ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake. Hili ni lazima tulisimamie hata wakati tunapoona hisia zetu zinaumizwa na uovu.

Pichani kushoto mama Nuru Pinda akiwa na mtoto George mwenye Ualbino kutoka Chato huko Kagera ambaye familia ya Waziri Mkuu imechukua jukumu la kumlea.

Ni nini basi tufanye kupambana na suala hili la mauaji ya Albino. Naandika kwa kirefu mapendekezo yangu kwenye toleo la kesho (Jumatano) la Tanzania Daima.

CHECHE PEKEE

MAUAJI YA ALBINO NI AIBU YETU—MWAKYEMBE

Na. Mahmoud Rashid

Mbunge wa Kyela Mhe. Harrison Mwakyembe amesema kuwa matukio ya mauaji wa maalbino nchini ni aibu na fedheha kubwa kwa taifa na ametoa wito kwa Watanzania wote kushiriki katika kuyakomesha. Mhe. Mwakyembe (CCM) amesema hayo katika mahojiano na KLHN kwenye tovuti yetu ya mwanakijiji.com ambapo alizungumzia masuala mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Mhe. Mwakyembe alisema kuwa mauaji haya ya albino "ni kitu ambacho kinaudhi, kinakereketa na kinaiabisha nchi yetu". Akielezea juhudi anazofanya yeye kwenye jimbo lake kuhusu kuelimisha jamii kuhusu adha hii ya albino Bw. Mwakyembe amesema kuwa katika Jimbo lake na katika mikutano yake mbalimbali huko amewatahadharisha wananchi wa Kyela kuwa "akiguswa mtoto yeyote albino ni jamii nzima inahusika".

Alitoa msisitizo kwa wanasiasa wote na viongozi mbalimbali kulipa uzito na umuhimu wa pekee suala hili katika maeneo yao. "Kwa kweli hili ni aibu kubwa sana; sasa hivi tukienda nje ya nchi tunashindwa kutembea kwa fahari kama zamani kwani hili linatuabisha mno, sijui nikuambie nini".



Mhe. Mwakyembe

Pamoja na hayo Bw. Mwakyembe alitoa pongezi kwa serikali akitambua juhudi zinazofanywa na vyombo mbalimbali kukabiliana na mauaji haya ambayo yamesababisha matatizo na hofu kubwa kwa wananchi wenzetu ambao wana ukosefu wa chembe zinazotengeneza rangi mwilini (ualbino).

Mhe. Mwakyembe pia alizungumzia kauli ya Waziri Mkuu ambayo inadaiwa kutolewa na kutafsiriwa na vyombo na watu mbalimbali kuwa ni ya kuhalalisha wananchi kujichukulia sheria mikononi dhidi ya watuhumiwa watakaoshukiwa kuhusika na mauaji ya albino.

"Tunaye Waziri Mkuu makini sana na mwanasheria aliyebobea, ninampa benefit of the doub kuwa alichomaanisha ni kuwa adhabu ya watu wanaoua ni kifo kama ilivyo katika sheria zetu" alisema Mhe. Mwakyembe.

Zaidi ya hayo Mhe. Mwakyembe alifafanua kauli ambayo inadaiwa kutolewa naye kuhusu uanachama wake ndani ya CCM. "Niende upinzani, upinzani upi? Mimi nimejiunga CCM tangu TANU nikiwa kijana na ninazeekea CCM" Alisema.

Akifafanua kauli yake hiyo kuwa inamaanisha kuwa yeye hawezi kutoka CCM Mhe. Mwakyembe alisema kuwa yeye ni mtu aliyesoma na anajua ameingia kwenye siasa kutumia nchi yake na siyo kuganga njaa.

Aliwakejeli pia wanasiasa ambao ni wanachama wenzake kwenye CCM ambao wamekuwa wakitumia vyombo mbalimbali vya habari kujaribu kile alichokiita "kujisafisha" na "kuwachafua wengine".

Pamoja na hayo Mhe. Mwakyembe alizungumzia mambo mbalimbali yakiwemo masuala ya Richmond ambapo ametahadharisha kutotoa hukumu hadi Waziri Mkuu atakapotoa taarifa ya utekelezaji wa maamuzi ya Bunge.

Tembelea tovuti yetu ya http://mwanakijiji.com na usikilize mahojiano hayo siku ya Jumatano.

DA' JESSY: TANZANIA TUNAYOITAKA

Na. Jessica L Fundi



Matukio mengi ambayo bado yamo kwenye mawazo yetu yananilazimisha kuuliza swali ambalo bado sijapata jibu la kutosheleza.

Je na sisi tunaweza kujenga taifa la kisasa ambapo raia wake watakuwa na nafasi sawa ya kufanikiwa na kupewa ulinzi wote wa kikatiba bila kujali hadhi zao?

Kinachonisikitisha sana sasa hivi ni hisia kwamba tuna Tanzania mbili. Ipo Tanzania ya wale wenye nguvu, wenye fedha na wenye madaraka ambao wao walitakalo huwa na waliwazalo hutokea na ipo Tanzania ya wale wakesha macho na walalahoi wa nchi yetu.

Hii ni Tanzania ya kina mama ambao bado wanajitahidi kila kukicha kuinua maisha yao na ya familia zao na kina baba ambao kila siku inabidi wafikirie njia gani za mkato za kujipatia kipato kwani njia zile halali karibu zote zinamilikiwa na Watanzania wa kundi lile la kwanza.

Kwa wiki kadhaa tumekuwa tukipokea barua za mambo mengi yenye kuelezea hali hii hasa jinsi "Jengo la Wamachinga" linavyotarajiwa kugawiwa kwa watu mbalimbali.

Kuna hisia kubwa kati ya Watanzania walioko kwenye kundi la pili (wakiwemo Wamachinga) kuwa kuna uwezekano mkubwa wao nao wakawekwa wachache pale kama alama tu lakini wamiliki hasa watakuwa ni wale wale Watanzania wa kundi la kwanza.

Je hii ndiyo Tanzania tuitakayo? Je ni Tanzania hii ambayo tuliitaka tulipoamua kukataa utawala wa kikoloni na ule wa Sultani?



Majengo ya Machinga

Je hatukutaka uhuru wetu ili tuweze kujiamulia mambo yetu wenyewe na katika kufanya hivyo kujiamulia hatima ya maisha yetu sisi wenyewe pasipo vitisho au ulazimisho wa aina yeyote.

Je leo hii kweli miaka karibu 50 baadaye tuliyoijenga ndiyo Tanzania ile tuitakayo? Bado najiuliza.

Email: dajessy@klhnews.com

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...


KATUNI ZA WIKI

Picha ya Wiki



Ajali iliyoua watu 17 huko Arusha wiki iliyopita.





PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA

http://www.mwanakijiji.com

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia

KUTOKA KWENYE MTANDAO

Mimi nimamuunga mkono pinda kwa asimia mia, lakini kwa hilo zoezi tuanze na MAFISADI ambao wanaua watu wengi kuliko hao wauaji wa maalbino.— **Anon**

Lakini upande wa pili nimejaaribu kutafakari hivi, Pinda alikuwa na mtoto, mkewe au mwanae mwenye ulemavu wa ngozi na ameuawa kwa sababu tu ya ngozi yake. Kauli kama hiyo isingekuwa ngeni kwake na wala tusingekuwa tunaijadili hapa. Au Pinda angalikuwa mtoto wa yule baba(albino) aliyeuwawa juzi. Tusingekuwa tunaijadili kauli hii hapa.

Pamoja na kuwa sheria inapaswa kuchukua mkondo wake, Ikn stahili ya wauaji wa Albino ni kifo hilo halina mjadala, Hukumu aitoe hakimu, au Pinda bado stahili yao ni kifo—**Anon**

Kwa wanaomjua Pinda vizuri na hata wale wanafuatilia michango yake bungeni sidhani kama wanaweza kusimama kidedea kutetea kuwa hakusema maneno hayo. Huyu Mheshimiwa ana sifa ya kusema anachokifikiri bila kumung'unya maneno. Wakati mwengine inasaidia sana kuwa na kiongozi kama huyo lakini wakati mwengine ni hatari. Huu ndio mfano wake...

Nadhani itakuwa busara kwa Pinda kutoa ufafanuzi wa hili na pia kuonyesha uungwana wake kwa kukubali kuwa alikosea.— **TanzaniaNjema**

nadhani ushindi wa Obama umetufanya tuelewe zaidi wapi ambapo tunakosea na kuendelea kuwa nyuma katika kila nyanja. Ukiacha uwezo/umahiri wa Obama, inaelekea taratibu zetu na hasa Katiba yetu haiwezi kutusaidia kufikia malengo yoyote ya maana.—**Recta**

Hivi bila kwenda kuzungumza na wenzetu wa Japan tungepata wapi miradi hii? Wajapan wangelijua vipi kijiji cha Kengeja? Kijiji cha Kengeja na watu wake wanawahusu nini Wajapan? Bila kuwatambulisha watu hawa wa Kengeja, Wajapan wangewajua wapi? - **Rais Kikwete ziarani Zanzibar.**

TOA NAKALA MOJA

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mhariri@ klhnews.com

Tovuti: http://www.mwanakijiji.com

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*